HOTUBA YA FUPI YA KATIBU TAWALA MKOA WA PWANI DKT. DELPHINE MAGERE (PHD) WAKATI WA KUFUNGUA KIKAO KAZI CHA KUPITIA BAJETI ZA HALMASHAURI ZA MKOA WA PWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA CHALINZE TAREHE 29 JANUARI, 2021.

Katibu Tawala Msaidizi Serikali za Mitaa Ndugu Yona Mwakilembe;
Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu Ndugu Edward Mwakipesile;
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Chalinze Ndugu Ramadhan Possi;
Ndugu washiriki wa kikao kazi kutoka Halmashauri zote;
Mabibi na Mabwana

Awali ya yote, kwa kuwa wengi wenu ndiyo tunakutana leo kwa mara ya kwanza tangu mwaka huu wa 2021 uanze; na kwa kuwa bado tupo mwezi Januari, napenda kuwatakia wote heri ya mwaka mpya wa 2021. Namwomba Mwenyezi Mungu, mwaka huu wa 2021 uwe mwaka wa heri, Baraka, afya njema na mafanikio tele kwetu sote.

Baada ya salaam hizo za mwaka mpya, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutupa uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii hapa Chalinze tukiwa na afya njema. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atulinde na kututunza sote, katika kipindi chote tutakachokuwa hapa.

Ndugu Washiriki wa Kikao Kazi

Kikao kazi hiki ni muhimu sana, kwa sababu ni moja ya njia ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti.

Mipango na Bajeti ndiyo dira ya utekelezaji wa Halmashauri, ndiyo inayoelekeza na kuunganisha malengo ya Taifa na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Hivyo, ni dhahiri kuwa kuendelea kukosea kuandaa Mipango yetu kunachelewesha Halmashauri zetu kufikia malengo tuliyojiwekea kama Taifa.

Ndugu Washiriki wa Kikao Kazi

Naamini wengi wenu mnafahamu kuwa, ninyi ni watu wa muhimu sana kwa sababu ni sehemu ya Kamati ya Bajeti ya Wilaya, na ndiyo *think tank* ya Halmashauri. Kamati ya Bajeti inapaswa kuwa na uelewa mpana wa kuandaa Bajeti na uendeshaji Halmashauri ili iweze kumshauri Mkurugenzi na Madiwani kuhusu utekelezaji wa bajeti na uendeshaji mzuri wa Halmashauri.

Ndugu Washiriki wa kikao kazi

Kikao kazi hiki kinafanyika kikiwa kimejumuisha pamoja Maafisa Bajeti kutoka Halmashauri zote Tisa (9) za Mikoa wa Pwani. Napenda kutumia fursa hii ya uwepo wenu pamoja kubainisha maeneo kadhaa yenye kasoro au upungufu ili myafanyie kazi kabla ya kuwasilisha bajeti Hazina. Baadhi ya upungufu uliobainika wakati wa upitiaji wa bajeti zenu ni kama ifuatavyo:-

1. Kutoweka fedha za kutosha kulipia vikao vya kisheria vya Halmashauri kwenye chanzo cha fedha za uhakika;
2. Kutoweka fedha za kutosha kulipa posho na haki za Madiwani kwenye chanzo cha uhakika, jambo linaloweza kusababisha Madiwani kukosa posho;
3. Kutotenga fedha za kulipa madeni mbali mbali, yakiwemo ya watumishi;
4. Kutoweka fedha za miradi ya ujenzi kwa kupitia makusanyo ya ndani na badala yake fedha nyingi zinaonekana katika miradi lakini matumizi yake ni reccurent in nature;
5. Kutotenga fedha za kukamilisha miradi ya ujenzi Viporo, kupitia chanzo cha uhakika. Matokeo yake miradi mingi ya ujenzi kwenye Elimu na huduma za Afya imechukua muda mrefu sana kukamilishwa kama vile ujenzi wa nyumba za walimu na watoa huduma za afya, Mabweni, Maabara, Madarasa na Vyoo;
6. Kutoweka idadi inayotakiwa kwa watumishi wanaotakiwa kupata promosheni au kubadilisha kada na wakati mwengine kutozingatia Miongozo na vipaumbele sahihi;

7. Bajeti za Afya na Elimu kutojumuisha bajeti za vituo vya kutolea huduma katika ngazi za chini;
8. Kukosea kuchagua **GFS CODES** kwa Baadhi ya Malipo na Vyanzo vya makusanyo;

9. Baadhi ya idara na Vitengo kutoweka fedha kwenye kazi zake za Msingi (Mpango na Bajeti Kutozingatia mahitaji halisi ya idara au kitengo);
10. Idara ya Utawala, Kilimo, Mifugo na Elimu zina watumishi hadi ngazi ya chini lakini bajeti walizopanga hazioneshi kuzingatia watumishi hao, kiasi kikubwa cha fedha kimetengwa kuwezesha watumishi wa Makao Makuu ya Wilaya tu;
11. Mapato ya ndani ya Halmashauri Kuweka vyanzo vya mapato ambavyo siyo halisi kwa Halmashauri na kuweka kiwango kikubwa cha makusanyo.
12. Mapato ya ndani ya Halmashauri Kuweka takwimu kubwa kwenye chanzo ambacho siyo rahisi kukikusanya.
13. Baadhi ya Halmashauri kutoingiza vyanzo vyote vya mapato ikiwa pamoja na vyanzo lindwa (Protected source: mapato ya Hospitali na ada za shule)
14. Baadhi ya Halmashauri kutoweka Bajeti ya chanzo cha mapato ambacho kinategemewa kukusanywa.
15. Kutoweka fedha za kuendesha POS yaani fedha za kununulia vifurushi

Ndugu Washiriki wa kikao kazi

Ni matumaini yangu kuwa mtazitumia vizuri hizi siku tano (5) zilizopangwa kuchambua mipango na Bajet vizuri. Kila Halmashauri ihakikishe kuwa inakamilisha na Kutoka na Mpango na Bajeti nzuri. Nieleze azi hapa kuwa, sitaraji kutokea kasoro zozote, zikiwemo nilizobainisha hapo juu.

Aidha, napenda kupitia kikao hiki, kuagiza yafutayo:-

1. Maandalizi ya Mipango na Bajeti yazingatie Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la 12 tarehe 13 Novemba, 2020;

2. Maafisa Mipango wote wahakikishe wanapitia kikamilifu Mipango na Bajeti za idara na Vitengo vyote na Kuziboresha pamoja na kuhakikisha bajeti za vituo vya kutolea huduma vya *Government lower levels* zinajumuishwa katika Mpango Mkuu wa Halmashauri;

3. Maafisa Utumishi wote wapiti bajeti za PE na kujiridhisha kama watumishi wote wenye sifa za kupandishwa madaraja (promosheni) wameingia kwenye Mpango na na vile vile wahakikishe kuwa Mpango wa ujazaji nafasi wazi umezingatiwa;

4. Kila Mweka Hazina ahakikishe kuwa anabainisha maeneo yaliyokuwa na changamoto katika kulipa na kuhakikisha yanarekebishwa katika Bajeti hii yam waka 2021/22;

5. Afisa Mipango na Mweka Hazina wapitie makisio ya Makusanyo ya mwaka chanzo kwa chanzo na kuweka makisio halisi kwa kila chanzo;

6. Katibu wa Afya wote wapitie Bajeti za Afya na kujiridhisha mambo yote muhimu yamewekwa katika vituo vya kutolea huduma za Afya;

7. Wataalamu wa kisekta toka Sekretarieti ya Mkoa wapitie bajeti ya kila Halmashauri na kutoa ushauri na kujiridhisha kama Halmashauri wamezingatia Ssera, Miongozo na Maelekezo ya kisekta kwenye maandalizi ya Bajeti.

Ndugu Washiriki wa kikao kazi

Napenda kuwasisitiza kutumia vizuri siku mtakazokaa hapa, na nawaagiza Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu na Katibu Tawala Msaidizi Serikali za Mitaa kunipatia taarifa ya utekelezaji wa kazi hii inayofanyika hapa.

Kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kusisitiza maelekezo yaliyotolewa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alipokuwa mkoani Geita, ambapo alisisitiza umuhimu wa kuchukua tahadhari kwa magonjwa mbali mbali ya kuambukizwa, ikiwemo corona. Nawaelekeza kuchukua tahadhari zote zinazotolewa na wataalamu wetu wa afya, mkiwa hapa Chalinze na hata mtakaporejea kwenye vituo vyenu vya kazi

Ndugu Washiriki wa Kikao Kazi, Mabibi na Mabwana, baada ya kusema hayo, ninayo furaha kutamka kwamba kikao Kazi hiki kimefunguliwa rasmi.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza na nawatakia safari njema mtakapokuwa mnarudi kwenye vituo vyenu vya kazi.

Asanteni.